"Together we protect and promote Public Health"

kwa pamoja tunalinda afya ya jamii

TMDA
Tanzania Medicines & Medical Devices Authority

Jarida

Toleo Na. 12 | Aprili 2023

KAMATI YA BUNGE YA TEMBELEA OFISI ZA TMDA ZA KANDA YA KASKAZINI NA KANDA YA ZIWA

MAB YAPONGEZA MIFUMO YA UDHIBITI KATIKA VITUO VYA FORODHA

Yaliyomo

MAELEZO YA AWALI YA MKURUGENZI MKUU

Ninayo furaha kubwa kuwasilisha kwako toleo letu la 12 la Jarida hili ambalo ni mwendelezo wa lile lillowasilishwa kwenu mwaka jana. Kama kawaida, toleo hili linaongelea baadhi ya mafanikio na hatua muhimu za udhibiti wa usalama, ubora na ufanisi wa dawa, vifaa tiba, vitendanishi na bidhaa za tumbaku.

Miongoni mwa mambo mengi yaliyomo humu, toleo hili lina habari juu ya namna TMDA ilivyokamata watu wanaojihusisha na magenge ya utengenezaji na usambazaji wa dawa bandia. Ikumbukwe kwamba uingizaji wa dawa bandia sio tu kwamba ni uvunjifu wa sheria, bali pia ni uhalifu dhidi ya maisha ya binadamu.

Jambo lingine zuri lilipo humu linahusu tathmini ya kina iliyofanywa na timu ya wakaguzi wa Shirika la Afya Duniani (WHO) ambao walitembelea TMDA kufanya kazi hiyo ya ulinganishaji upya wa mifumo ya TMDA endapo inaendelea kukidhi mifumo ya udhibiti ya kimataifa.

Aidha, toleo hili pia linaangazia masuala mengine muhimu ikiwa ni pamoja na tathmini ya utendaji wa maabara hamishika za TMDA, tathmini ya mwisho ya mradi wa PAVIA na mafunzo ya wakufunzi kuhusu ufuatiliaji na utoaji taarifa za madhara yanayoweza kutokea kutokana na matumizi ya Chanjo (AEFIs).

Makala nyingine zilizomo katika chapisho hili ni pamoja na ziara Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Ustawi wa Jamii katika ofisi za TMDA kanda zilizopo Mwanza na Arusha sanjari na na ziara ya Wajumbe wa Bodi ya Ushauri ya Wizara katika vituo vya forodha vilivyopo Magharibi mwa nchi yetu.

Kando na mafanikio mengine makubwa yaliyofikiwa, toleo hili pia lina taarifa za anuwai za kusisimua ikiwa ni pamoja na namna Mamlaka inavyofanya kazi kwa weledi ili kuvutia wawekezaji wa viwanda vya dawa nchini, tuzo ambazo TMDA imepokea kwa kuwa na mifumo bora ya kieletroniki ya utoaji huduma katika mazingira rafiki ya biashara pamoja na Tuzo za Umahiri wa Uhusiano wa Umma ya mwaka 2022 katika utoaji wa programu bora za elimu kwa umma.

Kwa muhtasari, Toleo hili la 12 linaonesha idadi ya shughuli muhimu ambazo ni za kuvutia na kuongeza uelewa wa msomaji.

Nakutakia usomaji mwema!

Adam M. Fimbo
MKURUGENZI MKUU

Adam M. Fimbo
MKURUGENZI MKUU

TAHARIRI

Ndugu mpendwa msomaji,

Ninayo heshima kubwa kwa mara nyingine kuwasilisha Jarida la TMDA toleo la 12. Ni zaidi ya muongo mmoja sasa, tumekuwa tukichapisha Jarida hili kama sehemu ya juhudi zinazoendelea za TMDA za kutoa taarifa mbalimbali za udhibiti kwa wadau wetu wapendwa, ikiwa ni pamoja na wewe msomaji.

Utii wa hiari wa matakwa ya sheria ya TMDA ni pamoja na kuwa na taarifa za kutosha na za mara kwa mara za kiudhibiti kwa wadau katika kurahisisha na kufanikisha kazi za udhibiti. TMDA imekuwa ikichapisha Jarida hili ili kuifikia sehemu kubwa ya jamii na kuongeza uelewa juu ya shughuli za udhibiti zinazofanywa ndani ya kipindi ambacho taarifa hii imetolewa.

Kwa uzito wa kipekee, napenda kumshukuru Mhariri Mkuu, Bw. Adam M. Fimbo ambaye pia ni Mkurugenzi Mkuu wa TMDA kwa usimamizi wake thabiti na uongozi mahiri katika kipindi chote cha uandaaji na uidhinishaji wa toleo hili.

Mamlaka ina kazi kubwa ya kulinda afya ya jamii ikiwa ni pamoja na kuendelea kutoa wito kwa jamii kuwafichua watu wasio waaminifu wanaojishughulisha na utengenezaji na usambazaji wa bidhaa za tiba ambazo ni duni na bandia katika soko hapa nchini.

Nachukua fursa hii, kukualika kusoma na kufuatilia taarifa zinazotolewa na TMDA kupitia njia mbalimbali za mawasiliano likiwemo jarida hili ili uweze kufahamu mambo mbalimbali yanayotendeka ndani ya Mamlaka katika kukuhakikishia usalama, ubora na ufanisi wa dawa, vifaa tiba, vitendanishi na bidhaa nyingine zinazohusiana na afya.

Unakaribishwa kutoa maoni, ushauri na mrejesho kupitia njia mbalimbali za mawasiliano ya taasisi ili kuboresha maudhui ya jarida hili.

Karibu usome kwa furaha!

Gaudensia Simwanza
MENEJA, MAWASILIANO NA ELIMU KWA UMMA

Gaudensia Simwanza
MENEJA, MAWASILIANO NA ELIMU KWA UMMA

BODI YA WAHARIRI

Kamati ya Bunge yatembelea ofisi za TMDA za Kanda ya Kaskazini na Kanda ya Ziwa

Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Huduma za Jamii na Maendeleo ilitembelea Ofisi za TMDA Kanda ya Kaskazini na kanda ya Ziwa zilizopo jijini Arusha na Mwanza ili kujionea shughuli mbalimbali za udhibiti zinazosimamiwa na TMDA kati ya tarehe 24 na 26 Septemba 2022.

Ziara hiyo iliyokuwa ya siku tatu ilimshirikisha pia Naibu Waziri wa Afya, Mhe. Dkt. Godwin Mollel (Mb) kwa niaba ya Waziri wa Afya, iliongozwa na Mwenyekiti wa Kamati hiyo ya Bunge, Mhe. Stanslaus Nyongo (Mb) aliyeambatana na wajumbe wengine 30 wa Kamati hiyo.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa TMDA, Bw. Adam M. Fimbo aliwasilisha taarifa ya utendaji katika Kamati hiyo tarehe 24 Septemba, 2022 katika ofisi ya TMDA - Kanda ya Kaskazini jijini Arusha.

Wakati wa ziara hiyo ya Kamati katika Kituo Jumuishi cha Mpakani cha Namanga (OSBP) kilichoko Arusha iliridhishwa na kazi nzuri za udhibiti za TMDA kwa kuweka mifumo bora ya udhibiti wa uingizaji bidhaa nchini na uchunguzi wa ubora wa dawa kwa kutumia Maabara Hamishika (Mini lab) kabla ya kuruhusiwa kuingia katika soko.

Kamati pia ilipata muda wa kuzungumza na wasimamizi wengine wa sheria katika kituo hicho cha Namananga OSBP kwa lengo la kujifunza ushirikiano uliopo baina ya taasisi nyingine za udhibiti ndani ya Serikali.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo Mhe. Stanslaus Nyongo (Mb) kwa niaba ya wajumbe, aliipongeza Mamlaka kwa kazi nzuri inayofanyika na kuishauri TMDA iendelee kufanya kazi kwa bidii ili kulinda afya ya jamii kwa kuwa watu wengi wanaweza kuwa katika hatari ya kupata madhara yatokanayo na matumizi ya bidhaa zisizofaa.

Aidha, Mhe. Nyongo alipongeza ushirikiano uliopo baina ya taasisi za Serikali zinazofanya kazi kwenye kituo cha Namanga OSBP ikiwa ni pamoja na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA), Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Mamlaka ya Nguvu za Atomiki Tanzania (TAEC), Maafisa afya, Mamlaka ya Afya ya Mimea (TPH), Jeshi la Uhamiaji na Jeshi la Polisi.

"Tumejionea jinsi TMDA ilivyojipanga katika kutekeleza majukumu yake hususani katika ukaguzi wa dawa kwenye kituo jumuishi cha Namanga, Arusha na Uchunguzi wa Maabara ya TMDA jijini Mwanza na tumeridhishwa na kile kinachofanywa na TMDA," alieleza Mhe. Nyongo.

Vilevile, Mhe. Nyongo aliishauri Mamlaka kuimarisha mifumo ya udhibiti ikiwa ni pamoja na kuongeza rasilimali watu zaidi kwenye vituo vya mipakani ikiwa na lengo la kuwahakikishia wananchi usalama wa wa bidhaa za dawa, vifaa tiba na vitendanishi vinavyoingia nchini.

Wakiwa jijini Mwanza, Wajumbe wa Kamati husika walifurahishwa na uwekezaji mkubwa wa vifaa vya kisasa katika Maabara ya TMDA jijini Mwanza ambayo inalenga katika kuwahudumia wananchi wa Kanda ya Ziwa na nchi jirani.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri (MAB), Bw. Eric Shitindi aliwashukuru Wajumbe wa Kamati hiyo kwa kufanya ziara husika ya kikazi katika ofisi za TMDA za Kanda na kuwahakikishia wajumbe wa Kamati kuwa Bodi itasimamia utekelezaji wa maagizo na maelekezo ya Kamati yaliyotolewa.

MAB yapongeza mifumo ya udhibiti katika vituo vya forodha

Bodi ya Ushauri ya Wizara ya Afya kwa TFDA (MAB) imeipongeza TMDA kwa uwekezaji wa mifumo ya udhibiti wa uingizaji nchini kwa bidhaa za dawa, vifaa tiba na vitendanishi kwenhye vituo vya forodha (PoE).

Pongezi hizo zilitolewa na Mwenyekiti wa MAB, Bw. Eric Shitindi katika ziara ya kikazi ya MAB iliyofanyika katika Ofisi za TMDA Kanda ya Magharibi kuanzia tarehe 06 hadi 10 Machi, 2023.

Katika ziara hiyo iliyojumuisha wajumbe wa Menejimenti, vituo vyote vya forodha vilivyopo katika mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora vilitembelewa ikiwa ni pamoja na hospitali za rufaa za mikoa, vituo vya uchunguzi wa dawa, matanuri ya kuchomea taka, mitambo ya kuzalisha gesi tiba na vituo vya huduma za uongezaji damu.

Bw. Shitindi aliipopngeza Menejimenti ya TMDA kwa juhudi inazofanya katika kusimamia na kuimarisha mifumo ya udhibiti wa bidhaa nchini. “Sisi kama Bodi Tumeridhishwa na mifumo ya udhibiti iliyopo ambayo inajumuisha ukaguzi wa mara kwa mara wa vituo vya forodha ili kudhibiti bidhaa za tiba zisizokidhi viwango, bidhaa bandia na zisizoruhusiwa kuingia nchini mwetu”. Bw. Shitindi Alisema

Katika ziara hiyo, wajumbe wa MAB pia waliweza kukutana na Wakuu wa Mikoa ya Kigoma, Tabora na Katavi kwa lengo la kufahamiana ambapo wakiwa mkoani Kigoma, Mkuu wa Mkoa huo Bw. Thobias Andengenye aliwapongeza wajumbe hao kwa kuendeleza ushirikiano uliopo kati ya TMDA na taasisi nyingine za udhibiti mkoani hapo na kuahidi kuendelea kushirikiana na Mamlaka katika kulinda afya ya jamii.

Katika hatua nyingine, Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Bi. Mwanamvua Mrindoko alimshukuru Mwenyekiti wa MAB na ujumbe wake kwa kutembelea Mkoa wa Katavi na kuahidi kuunga mkono kwa vitendo kazi zinazofanywa na TMDA.

Vile vile, Katibu Tawala wa Mkoa wa Tabora (RAS) kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa huo – Mhe. Balozi, Dkt. Batilda Buriani alitoa shukurani zake kwa Mwenyekiti wa MAB na wajumbe kwa kutembelea Mkoa wa Tabora. Alisisitiza kuhusu kudumisha na kukuza ushirikiano mzuri katika masuala yanayohusiana na majukumu ya TMDA na kwamba mkoa wake utaendelea kutoa ushirikiano katika kazi zinazolenga kulinda afya ya jamii.

Wajumbe wa Bodi ya Ushauri (MAB) ni pamoja na Mhe. Eric Shitindi (Mwenyekiti), Prof. Said Aboud, Prof. Appolinary Kamuhabwa, CPA Zaina Thabit, Bw. Daudi Msasi, Bi. Emma Lekashingo na Bw. Adam M. Fimbo (Katibu).

TMDA yashinda tuzo ya umahiri ya uhusiano wa umma

TMDA yawa mshindi wa pili katika Tuzo ya Umahiri ya Uhusiano wa Umma ya mwaka 2022 katika kundi la utoaji bora Elimu kwa Umma iliyotolewa na Chama cha Maafisa Uhusiano na Mawasiliano kwa Umma cha Tanzania (PRST) hapo tarehe 18 Februari, 2023 katika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Julius Nyerere, Dar es Salaam.

Tuzo hiyo ambayo ilipokelewa na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano na Elimu kwa Umma kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa TMDA Bw. Adam Fimbo baadaye ilikabidhiwa kwake jijini Dodoma, ambaye alipongeza na kushukuru kwa hatua hiyo.

Uratibu mzuri wa TMDA katika programu za elimu kwa umma ambazo zimeweza kuifikia sehemu kubwa ya jamii na kufikisha ujumbe uliokusudiwa ndiyo chachu kubwa ya Mamlaka kufikia mafanikio hayo.

Katika mwaka 2022 pekee, TMDA iliweza kufanya jumla ya mihadhara 392, maonesho 27, vipindi vya televisheni na redio 114, machapisho na vielelezo vya uelimishaji 31, taarifa kwa vyombo vya habari 23, uhuishaji taarifa za tovuti 1,098 na mikutano mitano (05) ya waandishi wa habari

Matumizi ya vituo vinne vikubwa vya televisheni ambavyo ni TBC-1, ITV, Clouds TV na UTV vinavyorusha vipindi vya TMDA na Jamii kwa dakika 30 mara mbili kwa wiki vimesaidia sana Mamlaka kuweza kuwafikia wananchi wengi katika maeneo ya mijini na vijijini.

Maoni yaliyokusanywa na TMDA kutoka kwa watu katika makundi mbalimbali ya kijamii waliohojiwa wakati kufanya programu za uelimishaji umma kwa njia ya mihadhara, walionesha kutazama na kuvutiwa na vipindi vya TMDA katika runinga hivyo kupendekeza kuwa vipindi hivyo kuwa endelevu kwa mwaka mzima kwa kuwa vinaelimisha umma kwa njia rafiki.

Lengo mkakati la elimu kwa umma la Mamlaka limekuwa likiwekwa katika kila Mpango Mkakati wa TMDA wa miaka mitano tangu kuanzishwa kwa Mamlaka mwaka 2003. Programu hizo za elimu zilizoratibiwa vyema zimekuwa zenye manufaa kwa jamii na kuisaidia Mamlaka kujinyakulia tuzo mbalimbali ndani na nje ya nchi.

Tanzania yavutia wawekezaji zaidi viwanda vya dawa nchini

Ubalozi wa Tanzania nchini Algeria ulizialika taasisi za Tanzania zilizoko katika sekta za afya kukutana na wawekezaji wa viwanda vya dawa na vifaa tiba nchini Algeria mwezi Oktoba 2022. Ziara hiyo ilifanyika wakati wa Maonesho ya Sita ya Wafamasia yaliyoandaliwa na Ubalozi wa Tanzania nchini humo.

Ziara hiyo ni sehemu ya jitihada zinazofanywa na Balozi wa Tanzania nchini Algeria - Meja Jenerali Mstaafu Jacob G. Kingu ambaye anafanya kazi kwa bidii kuwashawishi wawekezaji kuwekeza nchini Tanzania.

Katika hotuba yake ya ufunguzi, Balozi Kingu alisisitiza kuhusu umuhimu wa kukuza uchumi kwa kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora za afya zikiwemo dawa na vifaa tiba vya kutosha. “Miongoni mwa majukumu ninayofanya katika ubalozi wetu hapa ni kuhakikisha kuwa dawa na vifaa tiba vya kutosha vinapatikana nchini kwetu,” alidokeza Balozi Kingu.

Balozi Kingu alisema kwamba Ubalozi huo umekuwa ukihamasisha wawekezaji wa nje kutumia fursa zilizopo Tanzania kuwekeza katika viwanda vya dawa kwa kuwa uwezo wa viwanda vya ndani kwa sasa unachangia asilimia 10 hadi 20 tu ya mahitaji ya nchi.

“Mazingira ya uwekezaji nchini kwetu ni mazuri, tunachotilia mkazo kwa sasa ni kuelezea faida tuliyonayo kama nchi ya ukubwa wa soko,

uwepo kwa Bohari ya Dawa (MSD) kama wakala wa manunuzi ya dawa Serikalini sanjari na ukaribu wa nchi takribani nane (8) tulizopakana nazo katika ukanda wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na zilizoko kusini mwa Afrika (SADC). Mazingira haya yatawawezesha wawekezaji kuzalisha kwa wingi na kupata soko” Balozi Kingu alisisitiza.

Wakati wa hafla hiyo, wawekezaji watano (5) wa viwanda vya dawa walitembelewa ambao ni SOPHAL (SOPHAL Site 1, Site 2) Orion Lab, Groupe Industries SAIDAL na Biopharm.

Mkaguzi Mwandamizi wa Dawa wa TMDA, Bw. Paul Sonda alitoa shukrani za dhati kwa mwaliko uliotolewa kwa Mamlaka na kueleza kuwa hadi sasa TMDA haijasajili bidhaa yoyote kutoka katika makampuni ya Algeria. Katika maelezo yake alisema kuwa Tanzania ina fursa kwa watengenezaji wa dawa na vifaa tiba kutoka Algeria kuwekeza nchini. “Serikali ya Tanzania inafanya kazi kubwa ya kuboresha mazingira ya biashara ili kuwavutia wafanyabiashara kuwekeza nchini,” Bw. Sonda alisema.

Katika hatua nyingine, Mkurugenzi Mkuu wa makampuni ya viwanda vya dawa vya SOPHAL, Bw. Khalil Amry, alieleza kuwa baadhi ya makampuni ya dawa ya Algeria yameonesha nia ya kuwekeza nchini Tanzania. “Tumekuwa tukiwasiliana mara kwa mara na Ofisi ya Ubalozi, na wametualika kutembelea Tanzania wakati wa Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (Saba Saba). Tumejifunza mengi kuhusu mazingira mazuri ya uwekezaji biashara Tanzania, yametuvutia na tayari tumetuma maombi TMDA kwa ajili ya usajili wa bidhaa zetu,” alisema Bw. Amry.

TMDA: Mshindi wa pili miongoni mwa taasisi zenye mifumo bora ya utoaji huduma kielekroniki nchini

TMDA imeibuka mshindi wa pili na kuwa mfano wa kuigwa katika kundi la maeneo yanayokidhi Viwango na Miongozo ya Sheria ya Serikali–Mtandao (e-GA) kwa mwaka 2021/2022

Tuzo hiyo iliyotolewa na e-GA, ilikabidhiwa kwa TMDA na Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Deogratius Ndejembi jijini Arusha tarehe 8 Februari, 2023 wakati wa Kikao Kazi cha tatu cha Mamlaka ya Serikali-Mtandao.

Ushindanishwaji huo ulishirikisha wadau mbalimbali wa e-GA ambao wengi wao ni taasisi za umma na wadau wengine wakubwa na kujadili utekelezwaji wa maazimio yao kuhusiana na mafanikio na changamoto zinazoikabili tasnia ya TEHAMA katika utekelezaji wa mifumo ya kisheria yenye lengo la kuboresha huduma zitolewazo kwao za taasisi za umma.

Uamuzi wa kuwapata washindi ulikuwa wa ushindani mkubwa ambapo majaji wabobefu katika tasnia hiyo walishirikishwa kupitia uratibu wa e-GA kwa kuzishindanisha taasisi za serikali zinazotoa huduma mbalimbali kwa njia ya TEHAMA.

Matokeo ya umuzi huo ambayo yaliitambua TMDA kama moja ya taasisi chache za umma zenye mifumo bora kabisa ya TEHAMA nchini, yameendela kuibua shauku zaidi Mamlaka kutoa huduma zake kwa umahiri ili kulinda afya ya jamii.

ABREMA watembelea TMDA kujifunza udhibiti

TMDA ilitembelewa na wageni kutoka Mamlaka ya Udhibiti wa Chakula na Dawa nchini Burundi (ABREMA) walioongozwa na Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi hiyo Bw. Nduwayo Ildephonse kuanzia tarehe 17 hadi 19 Januari, 2023 ili kujifunza na kupata uzoefu wa namna TMDA inavyofanya kazi katika udhibiti wa bidhaa za dawa na tiba.

Wageni hao walijifunza kuhusu mifumo thabiti ya udhibiti, mifumo ya uhakiki ubora, mifumo ya tathmini na usajili wa bidhaa, taratibu za ukaguzi, udhibiti wa uingizaji na usafirishaji bidhaa nje ya nchi, uchunguzi wa dawa, udhibiti wa majaribio ya dawa, ufuatiliaji wa bidhaa katika soko, udhibiti wa vifaa tiba, usimamizi wa rasilimali watu na fedha na mikakati iliyopo ya kukuza viwanda vya ndani.

Akizungumza katika hafla ya kuhitimisha ziara hiyo, Bw. Nduwayo Ildephonse aliishukuru TMDA kwa mapokezi mazuri na kwa fursa ya kujifunza waliyoipata. Aliongeza kwa kusema kuwa timu yake imejifunza na kupata uzoefu, maarifa na uweledi mkubwa ambao utasaidia kuwajengea uwezo wafanyakazi wa ABREMA watakaporejea nchini Burundi.

Katika hatua nyingine, Mkurugenzi Mkuu wa TMDA, Bw. Adam Fimbo, aliwashukuru wageni kutoka ABREMA kwa kuchagua kuja TMDA kujifunza na aliwakabirisha kwa mara nyingine tena kuja kujifunza ikiwa watakuwa na uhitaji huo ambayo pia ni sehemu ya utekelezaji wa Hati ya Makubaliano (MoU) iliyosainiwa baina ya Mamlaka hizo mbili.

Vilevile, Bw. Fimbo aliupongeza ujumbe huo kwa dhamira na utayari walio nao kuimarisha Mamlaka ABREMA. Aliwahakikishia kuwapatia ushirikiano wa kutosha wa kiufundi ili kuboresha upatikanaji wa dawa kwa kuwa juhudi za pamoja zinahitajika ili kukabiliana na dawa duni na bandia kwenye ukanda Afrika Mashariki.

TMDA yaidhinisha miongozo ya udhibiti bora na usimamizi

TMDA ilikamilisha na kuidhinisha miongozo mipya inayohusu "Mbinu Bora za Udhibiti wa bidhaa za dawa" na "Mifumo Bora ya usimamizi" mwezi Machi, 2023 Nyaraka hizo zimetengenezwa ili kuimarisha juhudi zilizopo za Mamlaka katika kuboresha utendaji kazi na kuhakikisha kwamba dawa na vifaa tiba vilivyopo katika soko ni bora, salama na zenye ufanisi kwa umma.

Mkurugenzi Mkuu wa TMDA, Bw. Adam Fimbo ameeleza kwamba miongozo hiyo ya mbinu Bora za Udhibiti itawasaidia wadau kukidhi matakwa bora ya udhibiti (GRPs) ili kuendeleza umahiri wa WHO katika kiwango cha ngazi ya 3 (ML-3) ili kuwa na udhibiti bora wa bidhaa hizo.

TMDA ilifikia kiwango cha ukomavu cha Ngazi ya 3 ya WHO (ML-3) tangu mwezi Novemba 2018 na kuwa Mamlaka ya kwanza ya Udhibiti barani Afrika kupata utambuzi kama huo. Mafanikio haya yalipatikana kutokana na TMDA kuwa na Mipango ya Maendeleo ya Kitaasisi (IDPs) na kuitekeleza kama ilivyopendekezwa na timu ya wakaguzi wa WHO mwezi Mei 2018.

Aidha, miongozo ya GRP iliyoidhinishwa itasaidia kwa kiasi kikubwa kupata ufumbuzi wa changamoto za udhibiti kama vile utandawazi wa masoko, ukiritimba wa michakato ya ugavi na matumizi mazuri ya rasilimali chache za kimataifa zilizopo.

Aidha, miongozo ya Usimamizi Bora husaidia Mamlaka zingine za Kitaifa za Udhibiti (NRAs) kufanya maamuzi madhubuti. Miongozo hiyo huelekeza kupata mbinu za matumizi mazuri ya rasilimali chache na utaalamu hivyo kupunguza kujirudia kwa kazi na kuharakisha michakato ya utoaji idhini.

Wazalishaji, wasambazaji,watumiaji na wadau wengine wa TMDA wanahimizwa kupitia miongozo iliyoidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji bora.



Doc No. TMDA/DMC/MRE/G/019
Rev.#00

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
MINISTRY OF HEALTH

TMDA

TANZANIA MEDICINES AND MEDICAL DEVICES AUTHORITY

GOOD RELIANCE PRACTICES

March 2023

TMDA Headquarters, Plot No. 56/1, Block E, Kisasa B Centre, Hombolo Road, P. O. Box 1253, Dodoma - Tanzania, Tel: +255 (26) 2961989/2061990/ +255(22) 2450512/2450751/2452108, Email: info@tmda.go.tz, Website: www.tmda.go.tz, Toll free: 08001100834

Toa taarifa ya madhara yatokanayo na kifaa tiba

Utoaji wa taarifa kwa hiyari za matukio yanayodhaniwa kusababishwa na matumizi ya vifaa tiba kupitia kwa wahudumu wa afya pia watumiaji wa bidhaa hizo ni muhimu katika kuisaidia TMDA kupata mrejesho kuhusu usalama na ubora wa vifaa tiba vilivyoko katika soko na kuchukua hatua stahiki.

Athari ya aina yoyote inayohisiwa kusababishwa na matumizi ya vifaa hivyo inapaswa kuripotiwa, Mamlaka ili kufanyiwa uchunguzi kabla kuondolewa katika soko.

Vifaa tiba ni vyombo, vifaa, mashine, kemikali au kitu chochote kifananacho na hivi kinachotumika katika kutibu, kutambua, kupima, kuchunguza au kuzuia magonjwa ya binadamu au mifugo.

TMDA inawahimiza wananchi na watoa huduma za afya kuripoti tukio lolote linaloshukiwa kutokea baada ya matumizi ya kifaa tiba kwa kujaza FOMU YA RANGI YA CHUNGWA inayopatikana kwenye tovuti ya

TMDA (https://www.tmda.go.tz/publications/97) au katika kituo cha kutolea huduma za afya kilicho karibu, duka la dawa, ofisi ya Mganga Mkuu wa Wilaya, ofisi ya Kanda ya TMDA au katika kituo cha kukusanyia taarifa za madhara.

Pia Mamlaka inatumia njia nyingine za utoaji taarifa ikiwa ni pamoja na nyenzo ya kielektroniki ya kurahisisha upokeaji taarifa za madhara au matukio husika kupitia https://sqrt.tmda.go.tz. Kupiga simu bila malipo 0800110084 au kubofya namba *152*00#.

Kuripoti tukio linatokana na madhara ya kifaa tiba itasaidia kulinda afya ya jamii.



TMDA yazindua maabara mpya ya uchunguzi wa vifaa tiba na vitendanishi

Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba Tanzania (TMDA) imezindua maabara yake mpya mahususi kwa ajili ya uchunguzi wa vifaa tiba na vitendanishi jijini Dar es Salaam. Vifaa vya maabara hiyo mpya vya kisasa vyenye thamani ya shilingi milioni 250 vimefungwa katika maabara hiyo ili kuongeza wigo wa huduma za Mamlaka za uchunguzi wa vifaa tiba na vitendanishi. Baadhi ya vifaa vilivyowekwa ni pamoja na hadubini za LED, majokofu, makabati ya usalama a viumbe hai, mashine za Centrifuge naThermocycler.

Maabara ya Uchunguzi wa vifaa tiba huchunguza uwezo wa utendaji kazi wa vipimo vya haraka kwa magonjwa ya binadamu (RDT) na kuhakiki bidhaa hizo endapo zinafanya kazi kwa usahihi na ufanisi.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo wa maabara hiyo, Bi. Catherine Luanda ambaye ni Kaimu Meneja wa Uchunguzi wa Vifaa Tiba na Vitendanishi wa maabara hiyo alisema kuwa uwepo wa vifaa hivyo vipya ni muhimu na utaharakisha uchunguzi wa bidhaa za wateja wa Mamlaka.

"Uwepo wa vifaa vya kisasa vya maabara ni muhimu katika maabara yoyote ile na itasaidia kwa kiwango kikubwa katika uchunguzi na kupata majibu ya kuaminika," Bi Catherine alisisitiza.

Aliendelea kueleza kwamba baadhi ya vifaa hivyo vitatumika kufanya uhakiki wa ufanisi wa vipimo vinavyotoa majibu kwa haraka vya Malaria, UKIMWI, Kaswende na ubainishaji wa mimba kupitia mkojo.

Vitendanishi humaanisha kifaa kinachotumika pekee au pamoja na vifaa vingine kama ilivyokusudiwa na mtengenezaji kwa uchunguzi wa magonjwa binadamu au mifugo .

Dawa za kupunguza maumivu na vijiuasumu zaongoza kuingizwa nchini

Takwimu zilizopo za TMDA katika kanzidata zinaonesha kuwa takribani dawa za binadamu kiasi cha 13,000 zimeingizwa nchini Tanzania tangu 2020 ambapo bidhaa zenye viambato hai vya Acetylsalicylic Acid + Caffeine + Paracetamol zinaongoza katika orodha hiyo.

Dawa nyingine katika orodha ya tano bora kwa kuingizwa nchini ni pamoja na Ampicillin na Cloxacillin combination, Paracetamol, Magnesium + Aluminium + Simethicone na Goodmorning lung tonic.

Kaimu Meneja wa Usajili wa Dawa wa TMDA, Bw. Felchism Apolinary, alisema kuwa kiashiria cha dawa zinazoingizwa nchini kwa wingi kutoka nje ya nchi kwa miaka mitatu mfululizo iliyopita humaanisha kwamba zinatumika

kwa wingi nchini.

Bw. Felchism alidokeza kwamba wawekezaji wananweza kuchangamkia fursa hiyo na kuwekeza ndani ya nchi kwa viwanda vya kuzalisha dawa au malighafi za kuzalisha dawa husika

Alifafanua kuwa, "Wawekezaji wanahimizwa kuwekeza kwa kiasi kikubwa katika sekta ya viwanda vya dawa kwani mazingira ya uwekezaji nchini Tanzania ni mazuri na soko ni la uhakika".

TMDA iko makini na imejipanga vyema kutoa msaada wa kiufundi katika ngazi zote za uwekezaji nchini Tanzania hususani kwa wawekezaji wanaopenda kuwekeza katika viwanda vya dawa nchini, Bw. Felichism aliongeza.

TMDA kanda ya mashariki yaongoza kwa upimaji wa sampuli kupitia maabara hamishika (Mini-Lab kits)

Maabara ya Udhibiti Ubora ya TMDA ilianzishwa chini ya Kifungu cha 14(1) cha Sheria ya Dawa na Vifaa Tiba Tanzania, Sura 219 ili kufanya uchunguzi wa bidhaa zinazodhibitiwa. TMDA ina maabara tatu zilizopo katika Ofisi Ndogo ya Makao Makuu ya TMDA Dar es Salaam, Mwanza na Makao Makuu Dodoma. Maabara hizo zilizoanzishwa husaidiwa na vituo 25 vya Uhakiki wa Ubora (QACs) nchini.

Malengo ya QACs ni kukagua na kuchunguza aina ya kundi la dawa zilizopendekezwa katika vituo vya forodha kabla na baada ya kuingia katika soko la Tanzania. Aidha, hurahisisha ufuatiliaji wa ubora wa dawa zilizosajiliwa ili kulinda afya ya Jamii. QACs zote zilizoidhinishwa zina maabara hamishika kwa ajili ya kubaini bidhaa duni na bandia.

TMDA, ilisambaza maabara hamishika 25 katika hospitali 13 za rufaa za mikoa zilizopo Geita, Bukoba, Musoma, Manyara, Kilimanjaro, Mbeya, Katavi, Iringa, Lindi, Mtwara, Songea, na Bukoba. Nyingine 07 zipo katika ofisi saba za kanda za TMDA na tano (05) zipo katika vituo vya forodha vya Mtukula, Sirari, Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro, Namanga na Tunduma.

Tathmini ya utendaji kazi wa maabara hamishika zote 25 inaonesha kuwa maabara ya hamishika iliyopo Ofisi ya TMDA Kanda ya Mashariki, Dar es Salaam inaendela kufanya vizuri kuliko nyingine kwa miaka miwili mfululizo sasa. Mwaka 2021/22 iliweza kuchunguza jumla ya sampuli 719 na 617 hadi kufikia robo ya tatu (3) ya mwaka 2022/23. Tathmini hiyo pia inaonesha kwamba mwaka 2021/22 kituo kilichofanya vibaya ni Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Kigoma iliyochunguza sampuli tano (05) iliyopo katika nafasi ya pili kwa kufanya vizuri ni Ofisi ya TMDA Kanda ya Ziwa Mashariki iliyochunguza sampuli 478. Sampuli zinazoongoza kwa kuchunguzwa zaidi ni za dawa za Malaria, Kifua Kikuu, kufubaza makali ya virusi vya UKIMWI (ARVs) na dawa za kutuliza maumivu.

Mini Lab hurahisisha kuchunguza kwa haraka ubora wa bidhaa za dawa katika soko. Maabara za haina hii huweza kufanya uchunguzi na kubaini viwango vya viambato hai vilivyomo katika dawa husika, uwezo wa kuyeyuka kwa dawa zinazomezwa na kromatografia ya safu nyembamba (TLC) kwa ajili ya kutambua viambata hai vya dawa (APIs) vilivyopo kwenye dawa.

Ili kuthibitisha kuwa maabara husika 25 zinafanya kazi kwa ufanisi, TMDA imekuwa ikitoa mafunzo ya mara kwa mara kwa wataalam na kuhakikisha upatikanaji wa vitendanishi ikiwa ni pamoja na kufuatilia wa ukaribu utendaji wake kazi.

TMDA yatoa mafunzo kwa wakufunzi ya utoaji taarifa za madhara yatokanayo na matumizi ya chanjo kwa mikoa 10

Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba Tanzania (TMDA) imeendesha Mafunzo kwa Wakufunzi toka mikoa 10 juu ya ufuatiliaji na utoaji wa taarifa za madhara yanayoweza kutokea baada ya matumizi ya chanjo (AEFI) kwa washiriki 30 kuanzia tarehe 31 Januari - 3 Februari, 2023 mkoani Morogoro.

Mafunzo hayo ya siku nne yalilenga kuhamasisha na kuongeza uelewa kwa wakufunzi kutoka kwa watoa huduma wa afya wanaoripoti kuhusu AEFI.

Akifungua mafunzo hayo, Mkurugenzi wa Vifaa Tiba na Vitendanishi, Bi. Kissa Mwamwitwa aliwataka washiriki hao kuzingatia mada zinazowasilishwa kwa kuwa wanatarajiwa kuwafundisha maafisa wengine waliopo katika vituo vyao vya kazi.

"Ni matarajio yangu kwamba mtazingatia mafunzo yanayotolewa ili kufikia malengo yaliyokusudiwa na Mamlaka na hatimaye kuweza kufikia malengo ya Shirika la Afya Duniani (WHO) ya idadi ya taarifa 60 kwa madhara makubwa na 1,197 kwa madhara madogo ya AEFI kwa kila mwaka", Bi. Kissa alisema.

Washiriki hao 30 walitoka katika halmashauri mbalimbali kwenye mikoa 10 ambayo ni Arusha, Kilimanjaro, Mara, Simiyu, Njombe, Mbeya, Morogoro, Dar es Salaam, Iringa na Singida.

Taaluma za wa washiriki wa mafunzo hayo zilijumuisha Wafamasia wa Wilaya, Maafisa Chanjo wa Wilaya (DVOs), Waganga wafawidhi, Wafamasia wasimamizi, Wauguzi na wahudumu wengine wa kada ya afya.

TMDA imepanga kuongeza wigo wa mafunzo hayo ili kuwafikia wafanyakazi wote wa kada ya afya katika mikoa mingine iliyobakia ili kuhakikisha uwepo wa chanjo zenye usalama, ubora na ufanisi nchini.

"Ni matarajio yangu kwamba mtazingatia mafunzo yanayotolewa ili kufikia malengo yaliyokusudiwa na Mamlaka na hatimaye kuweza kufikia malengo ya Shirika la Afya Duniani (WHO) ya idadi ya taarifa 60 kwa madhara makubwa na 1,197 kwa madhara madogo ya AEFI kwa kila mwaka", Bi. Kissa alisema.

Jamii yaaswa kufichua wanaojihusisha na magenge ya dawa bandia

Jamii imeendelea kuaswa kuwafichua watu na magenge yanayojishughulisha na utengenezaji na usambazaji wa kinyemela wa dawa duni na bandia nchini kufuatia kukamatwa kwa Bw. William Japhet Mwangile (39) mkazi wa Kipawa - Dar es Salaam akitengeneza dawa bandia mnamo tarehe 14 Aprili, 2023.

Wito huo umetolewa na Mkaguzi wa Dawa wa TMDA Kanda ya Mashariki, Bw.Japhary Mtoro akiwa katika eneo la tukio na kuzungumza na waandishi wa habari mara baada ya kumkamata mtuhumiwa akitengeneza dawa bandia.

"Mtuhumiwa huyo alinaswa usiku wa manane maeneo ya Kipawa jijini Dar es Salaam ambapo alikutwa na lebo na vifungashio bandia vya dawa". Japhary alisema.

Bw. Japhary aliendelea kusema kuwa jumla ya lebo 537 za aina tofauti za dawa za Quinine sulphate, Erythromycin, na nyinginezo zilipatikana katika makazi ya mtuhumiwa huyo baada ya kufanyiwa upekuzi wa kina.

"Makasha matatu, moja likiwa na aina ya unga wa rangi ya njano na mengine mawili yakiwa na unga mweupe unaodhaniwa kuwa malighafi vilipatikana. Aidha, makopo 12 ya plastiki matupu yaliyotumika kupakia dawa hizo feki pia yalibainika na kutaifishwa". Bw. Japhary alifafanua zaidi.

Katika hatua nyingine, kiongozi wa Kitongoji cha Mtaa wa Matembele, Bi Maryglory Mambo aliyekuwa akishirikiana na TMDA na Jeshi la Polisi katika msako huo amewataka wananchi kuungana na TMDA ili kuwafichua watu wasio waaminifu wanaojihusisha na vitendo hivyo vya uhalifu.

Jamii imekumbushwa kuwa kusambaza dawa bandia ni uhalifu dhidi ya afya ya binadamu. Wahalifu wote wa namna hii lazima wapatikane na kuchukuliwa hatua za kisheria kwani wanahatarisha afya ya jamii. Aidha, jambo hili ni kosa kwa mujibu wa Sheria ya Dawa na Vifaa Tiba Tanzania, Sura 219.

"Makasha matatu, moja likiwa na aina ya unga wa rangi ya njano na mengine mawili yakiwa na unga mweupe unaodhaniwa kuwa malighafi vilipatikana. Aidha, makopo 12 ya plastiki matupu yaliyotumika kupakia dawa hizo feki pia yalibainika na kutaifishwa".Bw. Japhary alifafanua zaidi.

Baada ya miaka minne ya ngazi ya tatu (Ml-3) ya WHO: TMDA yatathminiwa upya

Kuanzia Desemba 2018 hadi sasa, TMDA inatambulika kwa kufikia kiwango cha Ngazi ya 3 ya Umahiri (ML3) cha Shirika la Afya Duniani (WHO) kwa kuwa na mifumo madhubiti na thabiti ya udhibiti wa ubora, usalama na ufanisi wa dawa. Kufikiwa kwa kiwango hicho kuliifanya Tanzania kuwa nchi ya kwanza barani Afrika kufikia daraja hilo.

Nafasi hiyo ilifikiwa baada ya kufaulu katika tathmini iliyofanywa na WHO katika mifumo ya TMDA ya udhibiti kwa kutumia nyenzo maalum ya kimataifa ya tathmini na upimaji (GBT). Nyenzo hii ni maalum kwa WHO kutathmini mifumo ya udhibiti wa ubora, usalama na ufanisi wa dawa na kuamua kiwango cha umahiri kwa taasisi za udhibiti za kitaifa duniani.

Tokea wakati huo, TMDA imekuwa ikiendeea ikiimarisha mifumo hiyo kwa kuzingatia viwango vya WHO na kuendelea kutoa huduma bora za udhibiti zenye ufanisi katika harakati za kukuza na kulinda afya ya jamii.

Baada ya miaka minne kupita, WHO iliifanyia tathmini TMDA kwa mara nyingine ambapo kati ya tarehe 27 na 31 Machi, 2023 ilituma timu ya wakaguzi 10 kuja TMDA kufanya kazi hiyo ikiwa ni njia ya ufuatiliaji na kuhakikisha kuwa viwango hivyo vinakuwa endelevu kwa lengo la kuhakikisha kwamba bidhaa za dawa na chanjo ni salama, bora na zenye ufanisi katika soko.

Tathmini hiyo ilifanyika kwa siku tano ambapo hoja zilizobainika ziliwasilishwa TMDA ili kupata majibu kabla ya kutangazwa rasmi na WHO ngazi ambayo Mamlaka imepata.

Mbali na TMDA, mamlaka nyingine za udhibiti barani Afrika ambazo zimepata ngazi ya WHO ML-3 hadi sasa ni pamoja na Mamlaka ya Chakula na Dawa ya Ghana (Ghana FDA), Wakala wa Kitaifa wa Usimamizi wa Chakula na Dawa ya Nigeria (NAFDAC), Mamlaka ya Dawa ya Misri (EDA) na Mamlaka ya Udhibiti wa Bidhaa za Afya ya Afrika Kusini (SAHPRA).

Mradi wa pavia waleta mafanikio katika utoaji taarifa za madhara ya dawa nchini

Mradi wa PharmacoVigilance Africa (PAVIA) ulifanyiwa tathmini ya mwisho ya utekelezaji wake kati ya tarehe 20 Agosti hadi 2 Septemba, 2022. Zoezi hilo lililenga kutathmini utekelezaji wa miradi yao inayofanywa kwa ushirikiano baina ya TMDA, Mpango wa Taifa wa Kifua Kikuu na Ukoma (NTLP), Taasisi ya Utafiti wa Dawa Kilimanjaro (KCRI) na Hospitali ya Kibong'oto (KIDH) nchini Tanzania. Wataalamu wa timu ya PAVIA waliohusika ni pamoja na Bi. Liza de Groot na Dkt. Edine Tiermesma wote kutoka KNCV na Dk. Linda Harmark kutoka Lareb, Uholanzi.

Tathmini hiyo ililenga katika utekelezaji wa kazi za ufuatiliaji wa usalama wa dawa na chanjo nchini Tanzania toka mradi huo ulipoanzishwa mwaka 2018 na unatarajia kukamilika mwishoni mwa mwaka 2023.

Nyenzo zilizotumika katika tathmini hiyo ni pamoja na mahojiano ya kina ya dodoso na mawasiliano ya teknolojia ya Zoom. Maeneo yaliyotathminiwa ni pamoja na vipengele vyote vya mfumo wa ufuatiliaji wa usalama wa dawa na chanjo katika ngazi ya kitaifa na kitaasisi, kanuni zilizopo, miongozo iliyoidhinishwa kwa utekelezaji, taratibu sanifu za utendaji kazi (SOPs) na nyaraka nyinginezo muhimu. Maeneo mengine yalihusu weledi wa rasilimali watu, vituo vya kutolea taarifa, miundombinu ya kutolea taarifa na viashiria vingine vya utendaji vinavyopima ufanisi wa ufuatiliaji.

Matokeo ya tathmini hiyo yameonesha mafanikio makubwa katika kuimarisha mfumo huo nchini. Wataalam wa kazi hiyo wa ndani wamejengewa uwezo mkubwa na walielimishwa kuhusu mfumo wa ufuatiliaji unaohusisha matukio yanayohusiana na utoaji wa taarifa za usalama wa dawa na chanjo. Taarifa za madhara ya dawa zilizoripotiwa zimepanda hadi 9,468. ikilinganishwa na taarifa 114 zilizokuwepo wakati mradi wa PAVIA ulipoanzishwa mwaka 2018 .

Mradi wa PAVIA unatekelezwa na Mamlaka za Udhibiti wa Dawa kutoka nchi nne (4) za Afrika ambazo ni Ethiopia, Eswatini, Tanzania, na Nigeria. Wadau wengine wa kimataifa wanaohusika na mradi huo ni Chuo Kikuu cha Verona (Italia), KNCV na Taasisi ya Maendeleo ya Afya Ulimwenguni ya Amsterdam (AIGHD), Uholanzi.

Bw. Mtani Njegere

Ilikuwa siku ya Jumapili tarehe 6 Novemba 2022, ambapo TMDA iligubikwa na majonzi baada ya kupokea taarifa za kushtusha juu ya kifo cha mfanyakazi wake mpendwa na ndugu - Bw. Mtani Njegere.

Kifo cha Bw. Njegere kilipokelewa kwa majonzi, simanzi, uchungu na masikitiko makubwa miongoni mwa wafanyakazi wa TMDA kwani alikuwa ni mtu mwenye upendo, mpole na mwenye utashi mkubwa.

Bw. Njegere alifariki dunia kufuatia ajali ya ndege ya Shirika la Precision Air ambapo watu 19 walipoteza maisha wakati ndege hiyo ilipoanguka katika ziwa Victoria wakati ikijaribu kutua katika uwanja wa ndege wa Bukoba.

Marehemu alijiunga na TMDA mnamo tarehe 2 Agosti, 2010 na alihudumu kama Mkaguzi wa Dawa kwa mud awa miaka 12 hadi tarehe 1 Aprili, 2022 alipoteuliwa kuwa Kaimu Meneja wa Majaribio ya dawa, nafasi ambayo aliitumikia hadi mauti yalipomkuta.

Marehemu Njegere alikuwa mchapakazi asiyetiliwa shaka, mtu wa kujituma na alijitolea katika kutekeleza majukumu yake ya kikazi.

Mchango wake kwa TMDA na taifa kwa ujumla utaenziwa daima.

ROHO YA BW. NJEGERE IPATE PUMZIKO LA MILELE MAHALI PEMA PEPONI AMINA

HABARI ZA KIJAMII

Hafla ya kuwaaga watumishi wastaafu wa TMDA tarehe 17 Septemba, 2023

MICHEZO KWA AFYA

Michezo kwa afya

OUR ADDRESS

@tmda_tanzania

@tmda_tanzania

@tmda tanzania

@tmda tanzania

Director General
Tanzania Medicines and Medical Devices Authority (TMDA)
P.O.Box 1253, Dodoma
P.O.Box 77150, Dar es Salaam
Tell:+255 222450512/2450751/2452108
Toll free: 0800110084
Email: info@tmda.go.tz
Websites: www.tmda.go.tz